**BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

70 Barabara ya Chukwani, Buyu
70490 Mjini Magharibi,
S. L. P 902 Chukwani,
Zanzibar, Tanzania

Simu: +255 24 224 2000
Nukushi: +255 24 224 2000
info@zanzibarassembly.go.tz
www.zanzibarassembly.go.tz

# HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA UTALII, BIASHARA NA KILIMO KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA KILIMO, UMWAGILIAJI, MALIASILI NA MIFUGO KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027.

**Mheshimiwa Spika,** Awali ya yote napenda nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu, Muumba wa Mbingu na Ardhi na vilivyomo ndani yake, kwa kutujaalia uhai na uzima na tukaweza kufika hapa leo hii ndani ya Baraza lako Tukufu na tukaweza kutekeleza majukumu yetu ya kitaifa. Namuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu anijaalie nguvu niweze kuwasilisha Hotuba hii na atupe usikivu na uelewa ili tuweze kuichangia kwa umakini na hatimae kuipitisha bajeti ya Wizara hii kwa maslahi ya Nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa dhati kabisa nachukua nafasi hii kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi pamoja na wasaidizi wake wote kwa kumsaidia vyema Mhe. Rais katika kutekeleza majukumu yake ya kuiongoza Nchi hii, pamoja na jitihada anazozichukua za kimapinduzi katika kuhakikisha analeta maenedeleo na mabadiliko ya kasi katika Sekta ya Kilimo.

**Mheshimiwa Spika,** Pia, napenda kuchua fursa hii kukushukuru wewe binafsi Mhe. Spika, Mhe. Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wa Baraza kwa namna mnavyoliendesha Baraza hili tukufu kwa umahiri mkubwa. Namuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu awazidishie busara pamoja na hekima katika kutekeleza majukumu yenu ya kutuongoza ili tuweze kutekeleza vyema wajibu wetu katika Chombo hiki muhimu kwa nchi yetu. Pia, tunaendelea kuipongeza wizara kwa mashirikiano waliyotupatia wakati wa kupitia Makadirio ya Bajeti ya Wizara hii.

**Mheshimiwa Spika,** Nitakuwa mwizi wa fadhila ikiwa sijawashukuru Wajumbe wa Kamati yetu kwa mashirikiano na umoja wao, kwa kazi nzuri waliyoifanya wakati wa kupitia Bajeti ya Wizara hii kwa ufanisi mkubwa, kwani tulikuwa bega kwa bega na Waheshimiwa Wajumbe hawa wakati wa kuyajadili makadirio na kuhoji mambo mbali mbali kwa lengo la kuhakikisha kwamba fedha zitakazoingizwa kwa Wizara hii zinakwenda kutumiwa kwa matumizi yaliyokusudiwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa heshima napenda kuwatambua Wajumbe hao kwa majina kama hivi ifuatavyo:-

| | | |
|---|---|---|
| *1.* | Mhe. Fatma Ramadhan Mohammed | Mwenyekiti |
| *2.* | Mhe. Dkt. Mohamed Ali Suleiman | M/Mwenyekiti |
| *3.* | Mhe. Abdulghani Ismail Zubeir | Mjumbe |
| *4.* | Mhe. Moza Mohamed Khamis | Mjumbe |
| *5.* | Mhe. Said Ali Juma | Mjumbe |
| *6.* | Mhe. Said Azana Hassan | Mjumbe |
| *7.* | Mhe. Juma Usonge Hamad | Mjumbe |
| *8.* | Ndg. Salha Abdulla Abdulla | Katibu |
| *9.* | Ndg. Himid Haji Choko | Katibu |
| *10.* | Ndg. Hafidh Ussi Haji | Afisa Bajeti. |

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inachukua fursa hii adhimu kumshukuru Mheshimiwa Fatma Mohamed Ramadhan, ambae alikua Mwenyekiti wa Kamati hii tokea kuundwa kwake hadi tunakamilisha maandalizi ya hotuba hii ambae kwa sasa anaendelea kutumikia Kamati nyengine. Vile vile Kamati inamkaribisha Mjumbe mpya katika Kamati hii Mheshimiwa Tabia Maulid Mwita, ambae nae kwa sasa anakuwa Mwenyekiti mpya wa Kamati yetu.

## MAKUSANYO YA WIZARA

**Mheshimiwa Spika;** Kamati inaipongeza Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kwa kufikia hatua nzuri ya makusanyo, kwani kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Wizara ilikadiriwa kukusanya **TZS Bilioni 8.241** na hadi kufikia Mwezi Machi 2026, imefanikiwa kukusanya **TZS Bilioni 6.272** sawa na asilimia 76% ya makadirio ya mwaka. Kamati inaamini kwa robo ya mwisho iliyobakia wizara inaweza kuvuka malengo ya ukusanyaji.

**Mheshimiwa Spika,** Pamoja na hatua hii nzuri ya ukusanyaji, lakini Kamati ilipochunguza katika kiambatanisho nambari 4 katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri, tumebaini kasoro katika Mapato ya Mashamba, ambapo makusanyo katika kianzio hicho yalikua ni asilimia 4% tu ya makadirio. Kamati ilipohoji suala hili iligundua kwamba, mapato haya yameshuka kwa kiasi kikubwa kutokana na kwamba sehemu kubwa ya mashamba hayo sasa hukodishwa na Msajili wa Hazina. Aidha, Changamoto nyengine ilibainika katika kianzio cha mauzo ya uzalishaji wa miche. Kamati ilihoji kushuka kwa makusanyo katika kianzio hicho na kuelezwa kwamba hali hiyo inatokana na uwamuzi wa Wizara wa kutoa

miche ya mikarafuu na minazi kwa wakulima bure ili kushajihisha kilimo cha mazao hayo.

**Mheshimiwa Spika;** Kamati inaishauri Wizara kukaa pamoja na Wizara ya Fedha na Mipango ili kuondoa changamoto iliyojitokeza katika kianzio cha mapato ya Mashamba kwa kuhakikisha kwamba makadirio ya mapato ya kianzio hicho yanawekwa kwa Taasisi au Wizara inayosimamia na kukusanya mapato hayo.

**Mheshimiwa Spika;** kwa mwaka wa fedha ujao 2026/2027 Wizara imepangiwa kukusanya jumla ya **Tzs Bilioni 12.13** kutokana na vyanzo vyake kwa Unguja na Pemba. Hivyo Kamati yetu inaishauri Wizara kuweka mikakati mahsusi ikiwemo kutoa mafunzo kwa watendaji, kutumia mifumo ya kisasa, kuziba mianya ya upotevu wa mapato na kuimarisha utowaji wa huduma bora na kwa wakati ili kuhakikisha inafikia malengo yaliyowekwa bila ya kuongeza gharama kwa wananchi.

## PROGRAMU ZA WIZARA

**Mheshimiwa Spika;** Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 imeanisha Programu Kuu nne. Kamati yetu inaunga mkono kuendelezwa kwa Programu hizo ambazo ni;-

1. Programu ya Utawala na Uratibu,
2. Programu ya Maendeleo ya Kilimo,
3. Programu ya Maendeleo ya Rasilimali za Misitu, na
4. Progamu ya Maendeleo ya Mifugo.

## PROGRAMU KUU YA UTAWALA NA URATIBU

**Mheshimiwa Spika,** Programu Kuu ya Utawala na Uratibu imepangiwa kutumia **TZS Bilioni 8.404** kwa Mwaka wa fedha 2025/202. Kamati inaishauri Serikali kuiangalia kwa undani zaidi programu hii kwa sababu uendeshaji wake unahitaji fedha za kutosha na ukizingatia programu hii haina mapato wanayoyategemea kwa sasa kwani pesa zote zinakwenda kwenye mfuko wa Mkuu wa Hazina.

## PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA KILIMO

Programu kuu ya Maendeleo ya Kilimo ina Programu Ndogo mbili ambazo ni Kuendeleza Miundombinu ya Umwagiliaji Pamoja na Maendeleo ya Huduma za Kilimo na Uhakika wa Chakula. Programu Kuu hii imepangiwa kutumia Tzs **Bilioni 147.731** kwa mwaka wa fedha 2026/2027. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuliongezea fedha fungu hili ukilingananisha na mwaka uliyopita wa fedha 2025/2026 ambayo ilikuwa ni **TZS Bilioni 49.392.**

Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kupatiwa fedha katika programu hii kama zinavyoombwa kwani Programu hii ina lengo la kuimarisha miundombinu bora ya umwagiliaji ambayo itapelekea kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula, kusimamia uzalishaji wa mbegu bora za nafaka, Kudhibiti miripuko ya maradhi ya mimea pamoja Kuimarisha hifadhi na upatikanaji wa chakula nchini kwa wakati wote na kupelekea kupungua kwa mfumko wa bei hasa wakati yanapotekea majanga mbalimbali duniani.

## PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA RASILIMALI ZA MISITU

**Mheshimiwa Spika,** Programu hii ina Programu Ndogo moja ambayo ni Maendeleo na Uhifadhi wa Misitu. Kiujumla maendeleo ya rasilimali za misitu Zanzibar yana mchango mkubwa katika maendeleo endelevu, kijamii na kimazingira. Programu hii kwa mwaka wa fedha 2026/2027 imepangiwa kutumia **Tzs Bilioni 11.945.**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Wizara kwa kushirikiana na mashirika mbali mbali kwa kuchukua hatua za kuilinda na kuendeza misitu ili kuhakikisha matumizi endelevu ya rasilimali hizi. Hata hivyo, Kamati inashairi wizara kuongeza kampeni za upandaji wa miti hasa ya matunda kwa kupitia wananchi, shule na taasisi za Serikali na binafsi ili kurejesha maeneo yaliyo haribiwa. Pia, Kamati inaishauri Wizara kuimarisha doria kwenye misitu kama vile, Msitu wa Jozani na Ngezi ili kuendelea kulinda dhidi ya watu wenye nia ovu.

## PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA MIFUGO

**Mheshimiwa Spika**, Programu ya Maendeleo ya Mifungu Zanzibar inaendelea kuimarika na ina nafasi kubwa katika kuongeza kipato cha wananchi na kukuza uchumi wa Taifa. Programu hii ina Programu Ndogo moja ambayo ni Uzalishaji na Utibabu wa Mifugo. Kwa mwaka ujao wa fedha Programu hii imepangiwa kutumia **Tzs Bilioni 13.735.**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa jitihada za kuimarisha Maendeleo ya Mifugo kwa uwekezaji mkubwa katika ujenzi unaendelea katika eneo la Karantini ya Mifugo Kisakasaka. Hata hivyo, Kamati inaishauri Wizara pamoja na mkandarsi kuongeza kasi ya ujenzi wa miundombinu ya mifugo unaondelea katika sehemu hiyo ili uwe na thamani halisi kulingana na fedha inayotumika hasa katika eneo la chelezo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati pia inaiihimiza Wizara kuwafuatilia wawekezaji pamoja na wananchi wote waliyolivamia eneo la karantini hiyo na kuhakikisha kwamba eneo hilo linarudi katika milki ya Wizara, na pia kusimamiwa kwa sheria na taratibu za Karantini za Mifugo zinazokataza maeneo hayo kuwa karibu na makaazi ya binadamu ili kujikinga na maambukizi ya maradhi ya wanyama.

**Mheshimiwa Spika**, Katika hatua nyengine, Kamati inashauri Wizara kuimarisha mashamba ya malisho ya mifugo, sambamba na kutoa elimu juu ya ufugaji wa kisasa ambao unafaida nyingi kulingana na soko liliopo ikiwemo kipato na ajira, chakula na lishe bora, pamoja na mbolea na kilimo.

**Mheshimiwa Spika,** Katika kuhakikisha wafugaji wetu wanapata tija na mafanikio ni lazima wapate utaalamu wa kutosha na technolojia ya kisasa badala ya kutumia njia za asili na mazoea. Katika kufuatilia suala hili Kamati yetu ilipata bahati ya kutembelea katika Kampuni ya AFI Green huko Kisarawe na Bagamoyo Tanzania Bara na kujionea shughuli za uzalishaji wa kuku. Kwakweli Kamati ilifarajika na njia na mbinu zinazotumika katika mashamba Darasa, njia ambazo ni bora na zinasaidia kupata vifaranga, kuku na mayai ambayo yanakidhi katika soko la ndani na nnje ya nchi yetu.

Kamati inaiomba Wizara na Serikali kwa ujumla kukamilisha michakato ya kuikaribisha Kampuni hiyo ambayo ni mdau muhimu katika myororo wa thamani ya mifugo, Kampuni ambayo inalengo la Kuanzisha Chuo cha Ufugaji kwa vitendo kwa wafugaji wa kuku wa hapa Zanzibar.

**HITIMISHO,**

**Mheshimiwa Spika,** Mwisho, napenda kuwashukuru na kuwapongeza tena Viongozi na Watendaji wa Wizara hii ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kwa juhudi wanazochukua katika kutekeleza kazi zao pamoja na ushirikiano wao kwa Kamati hii. Vile vile, nawashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwa kunisikiliza kwa utulivu wa hali ya juu wakati wote nilipokuwa nikiwasilisha hotuba hii.

**Mheshimiwa Spika,** Baada ya Maelezo hayo sasa niwaombe Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu waijadili, watoe ushauri pamoja na mapendekezo yao na hatimae waiunge mkono bajeti hii ili wamuwezeshe Mheshimiwa Waziri kufanikisha na kutekeleza yale waliojipangia katika mwaka wa fedha 2026/2027.

**Mheshimiwa Spika,** Baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. **Mheshimiwa Spika,** Naomba kuwasilisha.

**.........................................**

**(Mhe, Dkt Mohammed Ali Suleiman),**

**Makamu Mwenyekiti,**

**Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo.**

**BARAZA LA WAWAKILISHI,**

**ZANZIBAR.**